179 SIKU moja mavuno yataisha kabisa

179

1. Siku moja mavuno yataisha kabisa, baada ya hayo hukumu.
Jua litazimika siku hiyo ya mwisho, na hutasikia injili

> ***Refrain:***
> *Atakusanya ngano kwa furaha ghalani bali makapi yote yatatupwa motoni rafiki utakuwa wapi*

2. Mahubiri na nyimbo za wokovu wa mungu zitakaponyamaza huku,
uliyelikataa neno zuri la mungu, utakaa wapi milele

> ***Refrain:***
> *Atakusanya ngano kwa furaha ghalani bali makapi yote yatatupwa motoni rafiki utakuwa wapi*

3. Watu wote wa mungu wafikapo mbinguni kukaa pamoja na yesu,
wataimba kabisa kwa sauti nguvu kumshangilia mwokozi

> ***Refrain:***
> *Atakusanya ngano kwa furaha ghalani bali makapi yote yatatupwa motoni rafiki utakuwa wapi*
